

LUDOVICK Utouh



ANNE Makinda

# Wanaotaka CAG ang'olewe wanaijua Katiba?

NA EPSON LUHWAGO

**WIKI iliyopita, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ludovick Utouh, aliwasilisha Bungeni ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.**

Uwasilishaji huo ulifanyika kutokana na mamlaka aliyo nayo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa baada ya kukamilisha kazi hiyo ataipeleka kwa Rais na baadaye Bungeni.

Kama ilivyo ada, ripoti hiyo ya CAG imeibua madudu lukuki yaliyofanywa na watendaji wa serikali ikiwa pamoja na ubadhirifu wa mabilioni ya shilingi zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo.

Baada ya kutekeleza matakwa hayo ya kikatiba, umma wa Watanzania ulikuwa na shauku ya kujua kama wabunge ambao wanaendelea na mkutano wao mjini Dodoma, watajadili na kupendekeza ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa dhidi ya waliohusika kufanya madudu hayo.

Hiyo imekuwa kawaida kwa wabunge kupewa muda kujadili ripoti ya CAG na kwa kufanya hivyo kumekuwa na matunda kwani baadhi ya wahusika wamwekuwa wakiwajibishwa.

Miongoni mwa watu waliowajibishwa kutokana na utendaji au kuingia mikataba isiyo na tija kwa taifa ni vigogo wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), wakiongozwa na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu, Ephraim Mgawe.

Wengine waliokumbwa na rungu lililotokana na ugunduzi wa CAG katika ripoti zake ni aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Charles Ekerege na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Injinia William Mhando.

Mbali na vigogo hao wa mashirika ya umma, wapo mawaziri sita na manaibu wawili walioondolewa kwenye nyadhifa zao. Mawaziri hao na wizara walizokuwa wakiziongoza ni Dk. Cyril Chami (Viwanda na Biashara), William Ngeleja (Nishati na Madini), Ezekiel Maige (Maliasili na Utalii), Mustafa Mkulo (Fedha), Omari Nundu (Uchukuzi) na Dk. Hadji Mponda (Afya na Ustawi wa Jamii).

Naibu mawaziri waliokumbwa na kusambaratishwa na 'mafuriko' hayo ni Athumani Mfutakamba (Uchukuzi) na Dk. Lucy Nkya wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mawaziri hao na manaibu wao waliondolewa kutokana na shinikizo la wabunge baada ya kujadili ripoti ya CAG.

Inawezekana baadhi ya mawaziri hao hawakuhusika moja kwa moja na madudu hayo, lakini kwa kuwa watendaji wa taasisi zilizokuwa chini yao walihusika, walilazimika kuwajibishwa.

Kwa jumla, ripoti za CAG zimesaidia kurejesha nidhamu katika utendaji kazi serikalini pamoja na matumizi ya fedha hivyo kuwa kioo muhimu katika kutekeleza misingi ya utawala bora.

### WENGI WACHUKIZWA

Pamoja na kazi hiyo nzuri inayofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) chini ya CAG, kumekuwa na jitihada za kuikwamisha ili kutoa mwanya wa wajanja wachache kuendelea kunufaika na rasilimali za taifa na kuwaacha Watanzania walio wengi kuzidi kuwa katika umasikini uliotopea.

Juhudi hizo zinafanywa na baadhi ya watendaji wa serikali kwa kushirikiana na mtandao wa wanaofaidi rasilimali hizo huku wakitaka hata Bunge lisijadili ripoti hizo.

Ukweli juu ya hilo ni pale zilipoibuka taarifa kutoka Bungeni kwamba Ofisi ya Spika, baada ya kupokea ripoti hiyo, ilisema haitajadiliwa kama ilivyokuwa miaka mingine. Ofisi hiyo ilibaki kimya bila kusema kama itajadiliwa katika mkutano mwingine au la.

Hali hiyo imeleta minong'ono na maswali mengi yasiyo na majibu juu ya hatima ya ripoti ya CAG iliyobaini matatizo lukuki ya kiutendaji na ubadhirifu wa fedha za umma ambazo ni za walipakodi.

Wataalamu na wanasiasa, wakiwemo wabunge wenyewe kutokana na Spika wa Bunge, Anne Makinda, kunyamaza kuhusu ripoti hiyo wameelezea hali hiyo kuwa ni ya kutaka kukatisha tamaa juhudi za CAG za kuibua uozo unaofanywa na maofisa wa wizara, idara na taasisi za serikali.

Kwa mantiki hiyo, watu wana mtazamo kwamba Spika anashiriki (pengine bila kujua) kukwamisha mambo mazuri yanayofanywa na mwachuo mwenzake aliyesoma naye katika Chuo cha Maendeleo ya Uongozi (IDM), sasa Chuo Kikuu Mzumbe.

Baadhi ya wabunge wameshanganza na kitendo cha Spika na ofisi yake kuwa kimya bila kutoa tamko lolote. Pia wamedai kuwa katika kuonyesha kuwa kuna usiri uliogubikwa katika suala hilo, hata muda wa kujadili katika vikao vilivyopita ulipunguzwa.

"Hii ni kuonyesha kuwa kuna jambo la usiri lililojificha ndani yake na inawezekana uongozi wa Bunge unatumiwa na watu wanaotafuna mabilioni ya pesa za walipokodi kutokujadiliwa kwa ripoti ya CAG," alikaririwa Mbunge wa Ludewa (CCM), Deo Filikunjombe.

### MKAKATI KUMNG'OA CAG

Kama hiyo haitoshi, baadhi ya vyombo vya habari mwanzoni mwa wiki hii viliripoti kwamba kuna mkakati mzito wa kutaka Utouh aondolewe kwenye nafasi hiyo na kwamba mpango huo mahsusi unafanywa na baadhi ya watendaji wa serikali wanaodai ripoti zake zimekuwa zikiwaumbua!

Katika kufanya hivyo, kwa mujibu wa vyombo hivyo, Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Athanas Pius, ameshaondolewa kwenye nafasi hiyo na kuhamishiwa Wizara ya Fedha ambako atapangiwa kazi nyingine, huku mipango zaidi ikiandaliwa ili kumng'oa Utouh!

Inaonekana kwamba watu wanaofanya mpango huo hawajui madaraka na mipaka ya CAG katika kutekeleza majukumu yake. Kwa maneno mengine, watu hao ni mambumbumbu wa Katiba ya nchi.

Katika ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya 144 (1) inaeleza wazi kwamba CAG ataondoka katika nafasi yake anapofikisha umri wa miaka 60 ambao ndio wa kustaafu kwa lazima watumishi wote wa umma.

Pia Ibara hiyo hiyo kufungu (2) inabainisha kwamba: "CAG aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (asma kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, au kwa kuvunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma."

Kifungu cha 4 cha ibara hii kinaeleza kuwa Rais atamwondoa CAG iwapo tume iliyoundwa kuchunguza tuhuma zinazomkabili itaridhika kuwa ameshindwa kufanya kazi zake au kuwa na tabia mbaya. Iwapo itabainika kuwa tuhuma hizo ni za kwelie, basi tume hiyo itamshauri Rais kumwondoa CAG madarakani.

Kimsingi, kutokana na kazi anayoifanya, hata Rais Jakaya Kikwete alimsifu CAG na ofisi yake kwa jumla kwa kuwa ripoti zake zinapatikana katika muda unaotakiwa.

Kwa mantiki hiyo, CAG amefanya kosa gani hadi kusababisha kuwepo kwa mpango wa kumng'oa? Watu hao wanaifahamu Katiba au wanafanya mambo kwa utashi wao ili kutimiza matakwa yao ya kifisadi?

Kinachoonekana wazi ni kwamba watu hao wanaofanya hivyo wakidhani mbinu zao zikifanikiwa kumng'oa, maovu yao yatafichwa na umma hautajua chochote.

Ni vyema watu wanaosuka mpango huo wakidhani watafanikiwa wakafanya utafiti na kusoma Katiba kabla ya kufanya lolote. Kwa kufanya hivyo watajua mipaka na madaraka ya CAG ambavyo vimeainishwa ndani ya Katiba.